# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 6

# KISWAHILI PAPER 1 ANSWERS

1.Tawasifu

-Maelezo yanayohusu maisha ya mtu binafsi. Mwanafunzi/mtahiniwa aandike maelezo kuhusu maisha yake binafsi kuanzia kuzaliwa hadi alipo sasa. Arejelee:-kichwa kwa mfano,

TAWASIFU YANGU

TAWASIFU YA MIRIAM JUMA.

-Jina lake

-Tarehe,mwezi,mwaka

-Jambo lolote lisilo la kawaida lililoshuhudiwa kwake alipozaliwa

-Mwanambee,Mziwanda n.k

-Elimu yake kuanzia utotoni, kwa mfano shule ya chekechea,msingi na upili

-Changamoto alizokumbana nazo na namna alivyokabiliana nazo

-Mtazamo wake wa maisha

-Matarajio yake siku za usoni

-Mipango yake ya maisha n.k

Atoe maelezo yanayoonyesha umuhimu wake katika shule husika uliomfanya ateuliwe kuiwakilisha shule. Je,amekuwa kiongozi shuleni-ataje nyadhfa na mchango wake. Mapenzi yake kwa shule na matarajio yake kuihusu.

-Iandikwe katika nafsi ya kwanza

-Iandikwe kwa mtindo nathari/mfululizo

-Mpangilio uwe wa kiaya

-Hoja zipangwe ipasavyo

-Iwe na tamati KUTUZA

1.Atakayeandika insha yenye mtindo tofauti lakini ujumbe uwe wa tawasifu,akadiriwe ipasavyo kisha aondolewe maki nne sura (-4s).

2.Atakayekosa kuandika kichwa kamili,aondolewe maki mbili kichwa (-2k).

3.Atakayeandika insha tofauti kabisa, atakuwa amejitungia swali,atuzwe maki (D-0102.)

4.Atakayeandika wasifu atakuwa amepotoka.Atuzwe (D-01-02).

Insha ya mwanafunzi ishughulikiwe ipasavyo. Ni lazima arejelee uteuzi wake wa kuwakilisha shule katika kongamano.

2.Vijana-Watu wenye umri wa miaka kumi na minane hadi thelathini na mitano.Wa kike/wa kiume Changamoto-Jambo linalomkabili mtu.Si lazima afafanue maana ya maneno haya.

Changamoto zijumuishe;-

1) Ukosefu wa kazi

3) Ukosefu wa pesa za kujiendeleza

5) Utandawazi

7) Kuavya mimba

9) Shinikizo hasi la rika

11)Usherati/ukahaba

12) Ugaidi/mifano ya makundi kama Alshaabab

13) Kuvunjika kwa ndoa Hoja nyingine za wanafunzi zikadiriwe

KUTUZA

Insha sharti iwe na kichwa. Asiyeandika kichwa atozwe maki mbili kichwa (-2k) Insha iwe na utangulizi, mwili na tamati. Hoja za mwanafunzi ziwe tano au zaidi kumwezesha kuwekwa katika kiwango cha juu.

3.Hii ni methali.

Mwanafunzi atunge kisa kinachoafiki methali hii.

Maana ya methali,mtu anapotaka kupata/kufaulu katika jambo fulani ni lazima atie bidii.

Kuinama ni kule kutia kila aina ya juhudi katika jambo husika.

Visa vinaweza kurejelea;-

1.) Mwanafunzi aliyetia bidii masomoni akajinyima mambo mengi baadaye akapita mtihani.

2.) Mkulima aliyetia bidii katika kilimo akavuna mazao mengi.

3.) Mfanyakazi aliyetia bidii kazini akafanikiwa.

visa vinginevyo vikadiriwe ipasavyo.

Insha iwe na kichwa ambacho kinaweza kuwa methali hii au chochote kitakachokubaliana na kisa.Asiyeandika kichwa atozwe maki mbili kichwa (-2k) Insha iwe na utangulizi,mwili na tamati.

Mtahiniwa azingatie muundo wa methali nusu bin nusu; mathalan, Mtaka cha mvunguni-nusu

Sharti ainame-nusu

4. Hii ni insha ya mdokezo.

Mtahiniwa ayanakili maneno jinsi yalivyo kisha akamilishe kisa hicho kwa maneno yake.

Kisa kimhusu mwandishi/mtahiniwa (nafsi ya kwanza umoja).

Kisimulie tukio mbaya linalomkumba mhusika(mwandishi).

mama yake.

Awe aliyapuuza maonyo hayo na kuendelea na tabia mbaya inayomletea hali aliyomo sasa.

Aonyeshe dhana ya uchungu inayosababisha machozi kupuputika/kumdondoka.

Aonyeshe dhana ya majuto - kwa nini anajuta. Aonyeshe haja ya kurekebisha.

Visa vinaweza kuhusu;-

-Kufeli mtihani

-kuvamiwa usiku

-kuambulia uja uzito

-kushikwa/kupatikana katika kikundi haramu kama vile

Kijana yeyote aliyehusika katika vitendo haramu na kuhasirika.

Asiyeandika kichwa aondolewe maki mbili (-2k)

Atakayekosa kuanza kwa maneno haya atakuwa amejitungia swali.

amepotoka.

Atuzwe D-03 Asiyeonyesha maonyo, kujihusisha katika hulka mbaya na majuto vile vile atakuwa amepotoka.

Atuzwe D-03 Atakayesimulia kisa kinachomhusu mtu mwingine atakuwa amepotoka vile vile. Atuzwe D-03.